



Centrepay

Centrepay ni nini?

Centrepay—ni njia rahisi ya kulipa bili na gharama zako. Centrepay ni huduma ya kulipa bili kwa kujitolea ambayo haina malipo kwa wateja wa Centrelink. Tumia Centrepay kupanga makato ya kila mara kutoka kwenye malipo yako ya Centrelink.

Naweza kulipa bili gani na Centrepay?

Unaweza kulipa bili na gharama za kila siku kama kodi, gesi, umeme, maji na simu, pamoja na gharama nyingine za kwenye kaya.

Nitajuaje kama shirika au mtu amesajiliwa na Centrepay?

Unaweza kuwasiliana na shirika au mtu ambaye ungependa kulipa, ili kujua kama wamesajiliwa na Centrepay. Unaweza pia kuangalia kwenye humanservices.gov.au/centrepay kutafuta shirika au mtu ambaye ungependa kulipa.

Je, nianzisha makato ya Centrepay jinsi gani?

- Uliza shirika au mtu unayetaka kumlipa kama anaweza kuanza kupanga makato kwa ajili yako
- Kwenye mtandoni katika humanservices.gov.au/onlineservices
- utupigie simu kwa kutumia laini yako ya kawaida ya kulipia, au
- Uliza mojawapo ya vituo vyetu vya huduma.

Nahitaji kitu gani ili nianzisha makato ya Centrepay?

- Customer Reference Number (CRN) (Namba ya Marejeo ya Mteja) yako
- Maelezo kuhusu shirika au mtu unayetaka kulipia
 - jina
 - anwani na namba ya simu (kama inapatikana)
 - Centrelink Reference Number yao (namba hii inaanza na 555)
- Habari ya akaunti yako, kwa mfano akaunti yako ya umeme au nambari yako ya bili
- kiwango unachotaka kipunguzwe kutoka kwa malipo yako ya Centrelink kila wiki mbili, au kiasi kizima cha lengo unachotaka kulipa
- malipo ya Centrelink unayotaka vipunguzo kulipwa, na
- siku ya kulipa ambayo unataka makato ya Centrepay yaanze.

Anzisha makato yako ya Centrepay mtandaoni leo

Kuanzisha makato ya Centrepay mtandaoni lazima uwe na akaunti yako ya mtandaoni ya Centrelink ya sasa.

Ingia akaunti yako ya mtandaoni ya Centrelink kwa humanservices.gov.au/online au kupitia akaunti yako ya myGov.

Punde tu umeingia akaunti yako:

- chagua picha ya menu katika pembe la kushoto juu ya ukurasa

- chagua menyu ya 'Deductions' kwa upande wa kushoto, ndipo chagua 'View/Add/Change Deductions'
- chagua 'Add Centrepay or Tax deduction'
- punde umeingiza maelezo yote yanayohitajika, chagua 'Start Now'
- chagua aina ya makato unayotaka kuanza na chagua 'Continue'
- chagua 'Search for Service Provider'
- ingiza namba ya rejaleo ya mtoaji (namba hii inaanza na 555)
- maeneo yote yenye kinyota chekundu lazima yajazwe
- chagua mtoaji na chagua 'Continue'
- maeneo ya hiari yanapatikana kama ukitaka kuchagua tarehe ya mwisho au kiasi cha lengo. Makato yatasimama tarehe hii au wakati wa kufikia kiasi hicho
- punde tu habari zote zimeshaingiziwa chagua 'Continue'
- utaonyeshwa ukurasa wa 'Review and Submit'
- ikiwa habari zote ni sahihi, chagua 'accept the declaration' na chagua 'Submit'
- utapokea ujumbe kuhakikisha makato mapya yako ya Centrepay yameongezwa
- Uliza shirika kama makato ya kwanza ya Centrepay kimepokelewa. Unaweza kuangalia makato yako ya Centrepay mtandaoni ukitumia Express Plus app. Pakua mpako kutoka App Store na Google Play.

Wakati ukiwa mtandaoni kumbuka kufungua akaunti ya myGov ili kuunganisha akaunti yako ya mtandaoni ya Centrelink pamoja na huduma nyingine za serikali za mtandaoni.

Kwa habari zaidi

- angalia kwenye humanservices.gov.au/centrepay kwa maelezo zaidi katika Kiingereza
- angalia humanservices.gov.au/yourlanguage unapoweza kusoma, kusikiliza au kuangalia video vyenye maelezo ya lugha yako
- pigia simu nambari ya **131 202** ili kuongea nasi kwa kutumia lugha yako kuhusu malipo na huduma ya Centrelink
- pigia simu Translating and Interpreting Service (TIS National) (Huduma ya Utafsiri na Ukalimaniya Taifa) kwa **131 450** ili kuongea nasi ktika lugha yako kuhusu malipo na huduma ya Medicare na Child Support
- tembelea kituo cha huduma.

Muhimu: simu kutoka kwa simu yako ya nyumbani kwa namba za '13' kutoka mahali popote nchini Australia zinalipishwa kwa kiwango kimoja. Kiwango hicho kinaweza kutofautiana kutoka kwa bei ya simu ya eneo lako na huenda pia ikatofautiana kati ya watoaji wa huduma za simu. Simu kwa namba za '1800' kutoka kwenye simu yako ya nyumbani hazina malipo. Simu kutoka kwa simu ya umma na simu za mkononi zinaweza kupimwa muda na kulipishwa kwa kiwango cha juu.

Kanusho

Maelezo yaliyoko katika chapisho hiki yanakusudia kuwa mwongozo tu kwa malipo na huduma. Ni jukumu lako kuamua kama unataka kuomba kwa malipo na kufanya maombi na kulingana na hali yako maalumu husika.



Centrepay

What is Centrepay?

Centrepay—the easy way to pay your bills and expenses. Centrepay is a voluntary bill-paying service which is free for Centrelink customers. Use Centrepay to arrange regular deductions from your Centrelink payment.

What bills can I pay with Centrepay?

You can pay for bills and ongoing expenses like rent, gas, electricity, water and phone, as well as other household costs.

How do I find out if an organisation or person is registered with Centrepay?

You can contact the organisation or person you would like to pay, to find out if they are registered with Centrepay. You can also go to humanservices.gov.au/centrepay to search for the organisation or person you would like to pay.

How do I set up a Centrepay deduction?

- ask the organisation or person you want to pay if they can set up a deduction for you
- online at humanservices.gov.au/onlineservices
- call us on your usual payment line, or
- ask at one of our service centres.

What do I need to set up a Centrepay deduction?

- your Customer Reference Number (CRN)
- information about the organisation or person you want to pay
 - name
 - address and phone number (if available)
 - their Centrelink Reference Number (this number starts with 555)
- your account information, for instance your electricity account or bill number
- the amount you want deducted from your Centrelink payments each fortnight, or the total target amount you want to pay
- the Centrelink payments from which you want the deductions to be paid, and
- the payday that you want the Centrepay deduction to start on.

Set up your Centrepay deduction online today

To set up a Centrepay deduction online you must have an active Centrelink online account.

Log on to your Centrelink online account at humanservices.gov.au/online or through your myGov account.

Once you have logged on to your account:

- select the menu icon in the top left corner of the page

- select the 'Deductions' menu on the left hand side, then select 'View/Add/Change Deductions'
- select the 'Add Centrepay or Tax deduction'
- once you have entered all of the information required, select 'Start Now'
- choose the deduction type you wish to commence and select 'Continue'
- select 'Search for Service Provider'
- enter the reference number of the provider (this number starts with 555)
- all fields with a red asterisk must be completed
- select the provider and select 'Continue'
- optional fields are available if you want to select an end date or a target amount. Deductions will stop when this date or amount is reached
- once all details have been entered select 'Continue'
- you will be presented with a 'Review and Submit' page
- if all details are correct, 'accept the declaration' and select 'Submit'
- you will receive a message confirming your new Centrepay deduction has been added
- check with the organisation that your first Centrepay deduction has been received. You can check your Centrepay deductions online or with an Express Plus app. Download the app from the App Store and Google Play.

While you're online remember to create a myGov account to link your Centrelink online account as well as other government services online.

For more information

- go to humanservices.gov.au/centrepay for more information in English
- go to humanservices.gov.au/yourlanguage where you can read, listen to or watch videos with information in your language
- call **131 202** to speak with us in your language about Centrelink payments and services
- call the Translating and Interpreting Service (TIS National) on **131 450** to speak with us in your language about Medicare and Child Support payments and services
- visit a service centre.

Note: calls from your home phone to '13' numbers from anywhere in Australia are charged at a fixed rate. That rate may vary from the price of a local call and may also vary between telephone service providers. Calls to '1800' numbers from your home phone are free. Calls from public and mobile phones may be timed and charged at a higher rate.

Disclaimer

The information contained in this publication is intended only as a guide to payments and services. It's your responsibility to decide if you wish to apply for a payment and to make an application with regard to your particular circumstances.